

# CFA INSTITUTE TAARIFA YA HAKI ZA WAWEKEZAJI

"Taarifa ya Haki za Wawekezaji" ilitayarishwa na Taasisi ya CFA ili kuwashauri wateja wa huduma za kifedha kuhusu maadili na haki wanazofaa kutarajia kutoka kwa watoa huduma za kifedha. Haki hizi zinaonyesha kanuni msingi za maadili muhimu katika kuleta imani na kutegemeka katika uhusiano wowote wa kitaalamu. Orodha hii inatumika kwa bidhaa na huduma za kifedha kama vile usimamizi wa raslimali, utafiti na ushauri, huduma za kibinifsi za benki, bima na mali isiyohamishika. Iwe unaanzisha mpango wa kuwekeza, unashirikiana na ajenti, unafungua akaunti ya benki au unanunua nyumba, Taarifa ya Haki za Wawekezaji itakusaidia kupata maelezo unayohitaji pamoja na huduma unazotarajia na unazostahili. **Kuwataka wataalamu wa huduma za kifedha watii haki hizi hukusaidia kujenga imani kwa mtu au shirika unalojihusisha nalo na hivyo kurejesha imani, heshima na uadilifu katika taaluma ya fedha kwa pande zote husika..**

## NINAPOTAKA KUPOKEA HUDUMA ZA WATAALAMU AU MASHIRIKA YA FEDHA NINA HAKI YA...

1. Kuhudumiwa kwa **ukweli**, ustadi na maadili na kwa kutii sheria zinazohusika;
2. Kupokea ushauri na usaidizi huru na **usio na upendeleo** unaotokana na uchambuzi wa kina, ung'amuzi wa busara na juhudzi za dhati;
3. **Maslahi** yangu ya kifedha kupewe kipaumbele zaidi ya yale ya mhudumu na shirika;
4. Kuhudumiwa kwa **haki** sawa na wateja wengine;
5. Kuelezwawa kuhusu **mgongano wa maslahi** uliopo au unaoweza kutokea katika kutoa bidhaa au huduma kwangu;
6. Watoa huduma **kuelewa hali yangu**, ili ushauri wowote unaotolewa uwe wa kunifaa na kulingana na malengo na changamoto zangu za kifedha;
7. Kupokea **mawasiliano** sahihi, kamili, yanayoelewaka, yanayotolewa kwa muda unofaa, kwa lugha nyepesi na kwa mtindo unaowasilisha ujumbe inavyofaa;
8. Kuelezwawa kuhusu **ada** na gharama zote ninazotozwa na kupata maelezo ya kuonyesha kuwa gharama hizo ni za haki na zinafaa;
9. **Usiri** wa habari zangu;
10. Kupokea **kumbukumbu** sahihi na kamili kuthibitisha kazi ambayo imefanywa kwa niaba yangu.

Tembelea [cfainstitute.org/futurefinance](http://cfainstitute.org/futurefinance)